# هذه دعوتنا

# Hii Ndio Da´wah Yetu

**Imaam Muhammad Naaswir-ud-Diyn al-Albaaniy**

*Mfasiri:*

**Abu Bakr Khatwiyb al-Atrush**

بسم الله الرحمن الرحيم

**Ustaadh Ibraahiym:**

Alhamdulillah. Swalah za salaam zimwendee Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), na ahli zake na Maswahabah wake. Wa ba´ad:

Kwa hakika Allaah (Ta´ala) Ametuneemesha kwa neema ya imani, na Akauneemesha Ummah kwa kwa maulamaa (wanachuoni) ambao ndio waliokirimiwa na Allaah (Ta´ala) kwa kupewa elimu, ili (kutokana na elimu hio) wapate kuwaongoza watu juu ya njia ya Allaah, na juu ya njia ya ´Ibaadah ya Allaah (Azza wa Jalla). Na wao (wanachuoni) ndio warithi wa Mitume bila shaka yoyote. Sababu ya kujumuika hapa sisi – In Shaa Allaah, kwanza kabisa ni kumridhisha Allaah (´Azza wa Jalla), na pili ni kutafuta elimu ambayo itatufikisha katika hilo – In Shaa Allaah. Wallaahi, huu ni wakati wa furaha - kwa kukutana pamoja na Shaykh wetu, mwanachuoni wetu, na mwalimu wetu mkuu, Shaykh Muhammad Naaswir-ud-Diyn al-Albaaniy.

Kwanza kabisa - kwa niaba ya mkusanyiko huu tungelipenda kumkaribisha Shaykh wetu muheshimiwa, na kwa niaba ya kila anayesikiliza na khaswa wale watafutaji wa elimu, wote hao pia wanamkaribisha - nao wanatamani kujumuika leo pamoja na muheshimiwa mwalimu wetu. Na bila ya shaka, sote ni wenye shauku ya kusikia elimu na hekima aliyonayo. Kwa hivyo, tumsikilizeni kwa yale ambayo Allaah Aliyomneemesha nayo katika elimu. Kisha baada ya Shaykh wetu atapomaliza, hakika mlango wa maswali utafunguliwa, lakini maswali itabidi yaandikwe kwenye karatasi ambazo tutazigawanya – In Shaa Allaah. Tunarudia tena kusema, huu ni wakati wa furaha na tunasema karibu, kwa Shaykh muheshimiwa wetu.

**Shaykh al-Albaaniy:**

Ahlan bikum. Himidi zote ni Zake Allaah Tunamhimidi Yeye, tunamuomba Yeye msaada na tunamuomba Yeye msamaha. Tunajilinda kwa Allaah kutokana na maovu ya nafsi zetu, na kutokana na matendo yetu maovu. Yeyote Alieongozwa na Allaah, basi hakuna yeyote awezae kumpotoa. Na Yeyote Aliepotezwa na Allaah, hakuna yeyote awezae kumuongoza.

Nashuhudia ya kwamba hapana mola wa haki apasae kuabudiwa isipokuwa Allaah Mmoja, pasina mwenzi wala mshirika. Na nnashuhudia ya kwamba Muhammad ni Mtumwa Wake na ni Mtume Wake.

Amma ba´ad, kwa hakika bora ya maneno kabisa ni maneno ya Allaah, na uongofu bora zaidi ni uongofu wa Muhammad (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam). Shari ya mambo ni mambo ya kuzua, na kila kilichozuliwa (katika Dini) ni Bid'ah, na kila Bid'ah ni upotevu, na kila upotevu ni Motoni.

Namshukuru ndugu, Ustaadh Ibraahiym kwa maneno yake na kwa sifa zake, na mimi sina la kusema kwa hayo ila kufuata mfano wa Khaliyfah wa kwanza - Abu Bakr asw-Swiddiyq (Radhiya Allaahu 'anhu), ambaye alikuwa ndiye Khaliyfah wa kwanza wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) mstahiki. Pamoja na hivyo alipokuwa akimsikia mtu anamsifu kwa mambo ya kheri na akiamini ya kwamba sifa hizo, bila ya kujali anaemsifu hivyo, ameongeza chumvi - ilihali naye ni Khalifah wa Mtume wa Allaah, bi maana alizistahiki sifa hizo, lakini hata hivyo, [... Shaykh analia...] alikuwa akisema:

"Ee Allaah! Usinichukulie kwa wayasemayo, na nifanye bora kuliko wanavyonifikiria, na Unisamehe kwa yale wasiyoyajua."

Haya yanasema Bwana [Abu Bakr] asw-Swiddiyq. Je, tuseme nini sisi tuliokuja baada yake tusemeje? Mimi nasema nikifuata mfano wake:

"Ee Allaah! Usinichukulie kwa wayasemayo, na nifanye bora kuliko wanavyonifikiria, na Unisamehe kwa yale wasiyoyajua."

Hii ni haki niisemayo, mimi siye huyo mtu msifiwa ambaye mmemsikia hivi punde kutoka kwa ndugu yetu muheshimiwa Ibraahiym. Mimi si jengine mbali na kuwa mimi ni mtafutaji wa elimu (mwanafunzi). Ni juu ya kila mwanafunzi ashikamane na kauli ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) isemayo:

"Fikisheni kutoka kwangu hata kama ni Aayah moja. Na simulieni kutoka kwenye (hekaya) Baniy Israaiyl, kwani hapana madhara. Na yeyote anizuliae mimi uongo kwa kukusudia, basi ajiandalie makaazi yake Motoni."

Kwa hivyo, kwa kujiegemeza juu ya Hadiyth hii tukufu ya kiutume, pamoja na nususi zingine zilizoko katika kitabu cha Allaah na Hadiyth za Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam), tunajitwisha jukumu la kuwafikishia watu kwa yale ambayo huenda wakawa hawayajui. Lakini hii haina maana ya kwamba sisi ndio tumekuwa, kama yale yanayopatikana kwa baadhi ya ndugu zetu kutujengea dhana nzuri (ya kuwa sisi ni wakuu n.k). Sivyo kabisa! Huu ndio ukweli ambao uko ndani ya moyo wangu. Kila ninaposikia maneno kama haya, huwa nakumbuka mithali moja ya zamani maarufu ya wanachuoni, nayo ni:

*"Kwa hakika, kidege kwenye miji yetu kimekuwa tai."*

Baadhi ya watu hawatambui makusudio ya maneno haya au kwa mithali hii. *al-Bughaath* ni kijidege kidogo kisichokuwa na thamani yoyote, lakini kijidege hichi kidogo kikawa kama nusra kwa watu - hivyo ni kutokana na ujinga wao. Mithali hii ni ya kweli kwa wengi ambao wanalingania watu juu ya haki na uongofu au juu ya makosa na upotevu katika Uislamu. Lakini Allaah Anajua ya kwamba miji yote ya Kiislamu ni patupu, isipokuwa tu watu wadogo sana ambao, tunaweza kusema kuhusu wao ya kwamba "*Fulani ni mwanachuoni.*"

Kama ilivyokuja katika Hadiyth Swahiyh, iliyopokelewa na Imaam al-Bukhaariy katika Swahiyh yake kutoka kwa 'Abdullaah bin 'Amr Ibn al-'Aasw (Radhiya Allaahu 'anhu) kasema, amesema Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam):

"Kwa hakika Allaah Hatoinyakuwa elimu kutoka kwenye vifua vya wana-chuoni, lakini Ataichukuwa elimu kwa kuwaondoa wanachuoni, mpaka pasibakie mwanachuoni yoyote,... "

Hii ndio nukta yenyewe.

"... mpaka pasibakie mwanachuoni yeyote, watu watawachukuwa viongozi wajinga. Watawauliza maswali wafutu (kutoa fatwa) bila ya elimu. Basi wao watapotea na kuwapoteza wengine."

Anapotaka Allaah kuichukuwa elimu, hatoinyakuwa kutoka vifuani mwa wanachuoni, ikawa mwanachuoni ni kana kwamba ni mtu ambaye hajawahi kusoma hapo mwanzo. Hapana! Hii si katika Sunnah ya Allaah (´Azza wa Jalla) Afanyavyo

kwa waja Wake, na khaswa waja Wake wema - kuinyakuwa kutoka vifuani mwao elimu ambayo waliyojipatia kwa ajili ya kutafuta radhi za Allaah (Azza wa Jalla), kama mlivyosikia hivi punde kutoka kwa ndugu Ibraahiym - Allaah Ambariki - ya kuwa mkusanyiko huu tumekusanyika kwa ajili ya kutafuta elimu, Allaah (´Azza wa Jalla) ni Muadilifu Anaehukumu kwa uadilifu, Hainyakuwi elimu kutoka kwenye nyoyo za wanachuoni wa kikweli. Lakini Kajaalia ni miongoni mwa Sunnah za Allaah (´Azza wa Jalla) kwa viumbe Wake, Kuiondoa elimu kwa kuwachukuwa (kuwafisha) wanachuoni kwenda Kwake, kama Alivyofanya kwa Bwana wa wanachuoni, Manabii na Mitume wote, naye ni Muhammad (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam).

"... mpaka pasibakie mwanachuoni yeyote, watu watachukuwa viongozi wajinga, watawauliza maswali wafutu (kutoa fatwa) bila ya elimu. Basi wao watapotea na kuwapoteza wengine."

Hii haina maana ya kwamba Allaah (´Azza wa Jalla) Ataiacha ardhi bila ya kuwepo kwa mwanachuoni, ambaye kwa kupitia mwanachuoni huyo ndio Allaah Anawasimamishia hoja waja Wake, lakini maana ya hili, kila unapozidi kupita wakati elimu inazidi kupungua. Na zama zinavyokwenda hali itaendelea kuzidi kuwa namna hii ya mapungufu, mpaka pasibaki juu ya uso wa ardhi, mtu asemae: "Allaah, Allaah." Hadiyth hii mwaisikia mara nyingi, nayo ni Hadiyth Swahiyh:

"Hakitosimama Qiyaamah na juu ya uso wa ardhi (kukapatikana) mwenye kusema: "Allaah!, Allaah!"

Wengi miongoni mwa mfano wa watu hawa waliotajwa katika mwisho wa Hadiyth tulioitaja:

"... mpaka pasibakie mwanachuoni yoyote, watu watachukuwa viongozi wajinga,... "

Miongoni mwa watu hawa (wapotevu), ni wale wanaofasiri Qur-an na Sunnah kwa tafsiri zinazokhalifu na yale walivyofahamu wanachuoni, sitosema wale waliotangulia tu, bali hata wale waliokuja baada yao. Kwani hakika wanatumia Hadiyth hii ya "... Allaah, Allaah" kuzuju kwa, bali ya kupendekeza kumdhukuru Allaah (´Azza wa Jalla) kwa lafdhi ya mufradi: [yaani wanasema] "Allaah!, Allaah!" na kadhalika. Ili mtu yeyote asije kudanganyika au akawa hajui pindi anaposikia Hadiyth hii kwa taawili kama hizo, akaanza kufikiria kuwa ni jambo la sawa, kwanza nataka kuwakumbusha ndugu zetu waliohudhuria ya kwamba tafsiri hii ni batili. Jambo la kwanza, ni kwa vile kumekuja bayana yake [Hadiyth hii] katika upokezi mwingine kutoka kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam). Na jambo la pili, kwa kuwa tafsiri hii ingelikuwa ni sahihi, basi kungelikuwepo ishara katika matendo ya Salaf-us-Swaalih (Radhiya Allaahu ´anhum). Hivyo,

ikiwa wao hawakulifanya, basi ni dalili ionyeshayo ya kukataa kwao tafsiri hii ubatili (upotevu/uongo) wa tafsiri hii. Sasa itakuweje utakapoonyeshwa huyo upokezi mwingine, kama inavyosemekana kwamba Imaam Ahmad (Rahimahu Allaah) kaipokea Hadiyth hii katika musnadi wake kwa isnadi sahihi, kwa lafdhi:

"Hakitosimama Qiyaamah na juu ya uso wa ardhi (kukapatikana) mwenye kusema: "*Laa ilaaha Illa Allaah.*"

Hivyo basi, haya ndiyo makusudio kwa lafdhi (neno) Allaah kukaririwa, katika upokezi ule wa kwanza.

Nukta tuikusudiayo, katika ardhi (ulimwengu) leo - kwa masikitiko makubwa - wamewapuuza wanachuoni hao ambao walikuwa wakiujaza ulimwengu mzima kwa elimu zao na wakiieneza baina ya safu za watu wake, na leo imekuwa kama wasemavyo watu:

"*Ilikuwa wanapohesabiwa wanaonekana ni wachache, leo wamepungua kuliko ile idadi ya uchache waliokuwa nao.*"

Kwa hivyo, sisi tunataraji kutoka kwa Allaah ('Azza wa Jalla) Atujaalie ni miongoni mwa wenye kutafuta elimu (wanafunzi), ambao wanaoiga kutoka katika mifano ya wanachuoni kikweli kweli, na wanafuata njia yao kwa uaminifu. Hili ndilo tunalolitaraji kutoka kwa Allaah ('Azza wa Jalla) - Atujaalie ni miongoni mwa hawa watafutaji [elimu] wenye kupita njia hiyo ambayo kasema kuihusu Mtume wa Alllah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam):

"Yeyote mwenye kufuata njia kwa ajili ya kutafuta elimu, Allaah Atamsahilishia njia ya kuelekea Peponi."

Hili linanifungulia mlango wa kuzungumzia elimu hii, iliotajwa ndani ya Qur-aan sehemu nyingi sana. Kwa mfano kauli Yake Allaah (Ta´ala):

هَلْ يَسْتَوِي الَّذِينَ يَعْلَمُونَ وَالَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ

"Sema: Je, watakuwa sawa wale wanaojua na wale wasiojua?" **(az-Zumar 39 : 09)**

Na Kauli Yake (´Azza wa Jalla):

يَرْفَعِ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَالَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ دَرَجَاتٍ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ

"Allaah Atawainua wale walioamini miongoni mwenu, na waliopewa elimu (Atawainua) daraja za juu. Na Allaah Anazo khabari za mnayo yatenda." (al-**Mujadilah 58 : 11)**

Ni elimu ipi hii ambayo kutokana na elimu hiyo Allaah ('Azza wa Jalla) Kawasifia walio nayo na wakaitumia, pamoja na wale wenye kufuata njia ya watu hao? Jibu ni kama alivyosema Imaam Ibn al-Qayyim al-Jawziyyah (Rahimahu Allaah) ambaye ni mwanafunzi wa Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah):

***"Elimu ni ile ambayo: "Kasema Allaah", "Kasema Mtume Wake," na "Wamesema Maswahabah zake. Hili si uongo. Elimu si kuvamia kukhilafiana bila ya kuwa na mazingatio baina ya Mtume na baina ya rai ya Faqiyh (mwanachuoni). Hapana sivyo hivyo, na wala sisi hatuzikatai Sifa [za Allaah] na kuzipinga, kwa kuchelea tusije tukatumbukia ndani ya kuzifananisha na kuzipigia mifano [na sifa za viumbe]."***

Kwa hivyo, tunachukuwa kutoka katika maneno haya na mashairi haya - ambayo ni nadra kuyasikia katika maneno ya washairi, kwani mashairi ya wanachuoni si kama mashairi ya washairi. Mtu huyu (Ibn al-Qayyim) alikuwa ni mwanachuoni, na pia kaandika mashairi mazuri. Anasema:

***"Elimu ni ile ambayo: "Kasema Allaah".*** *Hii ni katika ngazi ya kwanza.* ***"Kasema Mtume wa Allaah".*** *Hii ni katika ngazi ya pili.* ***"Kasema Swahabah".*** Hii ni katika ngazi ya tatu.

Hapa ndipo ntaifanya kalima (mada) yangu kwa mashairi haya mazuri yenye baraka – In Shaa Allaah. Maneno ya Ibn al-Qayyim haya yanatukumbusha kuhusu uhakika (ukweli) ulio na umuhimu sana, ambao wameghafilika kwao (ukweli huo) wengi katika Madu´aat walioenea leo duniani kwa jina la Uislamu. Ukweli huo ni upi?

Jambo maarufu lijulikanalo kwa Madu´aat wote hawa ni kwamba [asili ya kulingania katika] Uislamu ni: "Kitabu cha Allaah na Sunnah za Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam)." Na hili ni jambo la haki lisilokuwa na shaka, lakini lina upungufu ndani yake. Upungufu huu ndio ambao kauashiria Ibn al-Qayyim katika mashairi yaliyopita. Ametaja baada ya Kitabu (Qur-aan) na Sunnah, kataja Maswahabah.

***"Elimu ni ile ambayo: "Kasema Allaah", "Kasema Mtume Wake," na "Wamesema Maswahabah zake."*** Mpaka mwisho [wa mashairi].

Siku hizi ni nadra sana kutokana na tunaowasikia mtu akisema: "Tunafuata Qur-aan na Sunnah" [kwa ufahamu wa] Maswahabah. Na kama tujuavyo sote, ya kwamba wao (Maswahabah) ndiyo walio katika kichwa cha Salaf-us-Swaalih (wema waliotangulia),

ambao kumepokelewa Hadiyth nyingi kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akiwazungumzia pale aliposema:

"Watu bora ni (wa) karne yangu,... "

Na usiseme kama wasemavyo wengi katika Madu´aat, wanasema:

*"Karne bora."*

Kusema: "Karne bora", maneno haya hayana asli katika Sunnah. Sunnah sahihi, kama ilivyo katika Swahiyhayn (al-Bukhaariy na Muslim) na nyinginezo katika marudilio ya Ahaadiyth na Sunnah, zimeitaja Riwaayah ya Hadiyth hiyo kwa lafdhi:

"Watu bora ni (wa) karne yangu, kisha wale waliokuja baada yao, kisha wale waliokuja baada yao."

Hawa Maswahabah ambao ndio wako nafasi ya mbele katika hizo karne tatu bora waliopewa ushuhuda wa kuwa ni bora, amewaunganisha Imaam Ibn al-Qayyim al-Jawziyyah katika Kitabu na Sunnah. Sasa huku kuunganisha kwake ilikuwa ni rai yake, ijtihadi yake [kama wanachuoni wengine] ambapo kuna uwezekano ya kutumbukia katika makosa. Jibu ni hapana! Haya hayatokani na makisio wala ijtihadi [ya uanachuoni] wake, jambo ambalo linaweza kupelekea ikawa ni makosa, bali [maneno yake] yameegemea juu ya Kitabu cha Allaah na Hadiyth za Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam).

Ama kuhusiana na Qur-aan, ni kutokana na kauli ya Mola wetu (´Azza wa Jalla) katika Qur-aan:

وَمَن يُشَاقِقِ الرَّسُولَ مِن بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُ الْهُدَى وَيَتَّبِعْ غَيْرَ سَبِيلِ الْمُؤْمِنِينَ نُوَلِّهِ مَا تَوَلَّى وَنُصْلِهِ جَهَنَّمَ وَسَاءَتْ مَصِيرًا

"Na atakayempinga Mtume baada ya kuwa umeshambainikia Al-Hudaa (Uongofu) na akaifuata njia isiyokuwa ya Waumini; Tutamgeuza alikogeukia (mwenyewe upotofuni) na Tutamuingiza (moto wa) Jahannam. Na uovu ulioje mahali pa kurejea." **(an-Nisaa 04 : 115)**

Mola wetu Hakuishia katika Aayah hii:

مِن بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُ الْهُدَى

"... baada ya kuwa umeshambainikia Al-Hudaa (Uongofu)... "

Na lau Angelifanya hivyo ingelikuwa ni haki.

yaani Hakusema:

*"Na atakayempinga Mtume baada ya kuwa umeshambainikia Al-Hudaa (Uongofu);... Tutamgeuza alikogeukia (mwenyewe upotofuni),"*

Bali Amesema, na hili ni kutokana na hekima kubwa - nayo ndio ambayo hivi sasa tuko mkuibainisha na kuifafanua. Kasema:

وَيَتَّبِعْ غَيْرَ سَبِيلِ الْمُؤْمِنِينَ

"... na akaifuata njia isiyokuwa ya Waumini... " **(an-Nisaa 04 : 115)**

وَمَن يُشَاقِقِ الرَّسُولَ مِن بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُ الْهُدَى وَيَتَّبِعْ غَيْرَ سَبِيلِ الْمُؤْمِنِينَ نُوَلِّهِ مَا تَوَلَّى وَنُصْلِهِ جَهَنَّمَ وَسَاءَتْ مَصِيرًا

"Na atakayempinga Mtume baada ya kuwa umeshambainikia Al-Hudaa (Uuongofu) na akaifuata njia isiyokuwa ya Waumini; Tutamgeuza alikogeukia (mwenyewe upotofuni) na Tutamuingiza (moto wa) Jahannam. Na uovu ulioje mahali pa kurejea." **(an-Nisaa 04 : 115)**

Natumai Aayah hii mtaizingatia vizuri katika fahamu zenu, na nyoyo zenu na wala nataraji hamtoisahau, kwa kuwa hiyo ni haki. Na kutokana na hilo [haki hiyo], mtaokoka na kupinda kuliani na kushotoni, na muokoke - hata katika suala moja tu - msije mkatumbukia katika moja ya mapote ambayo siyo yenye kunusuriwa; au moja ya mapote potevu. Hili ni kwa sababu Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) kasema katika Hadiyth maarufu, ambayo nitaifupisha ili tupate ile nukta ambayo twataka kuizungumzia:

"... na utagawanyika Ummah wangu katika makundi 73, yota hayo yataingia Motoni isipokuuwa kundi moja tu." [Maswahabah] wakasema: "Ni lipi hilo ewe Mtume wa Allaah?" Akasema: "Ni Jamaa´ah."

Jamaa´ah ni "Njia ya waumini." Kwa hivyo Hadiyth hiyo - ikiwa si Wahyi wa moja kwa moja kutoka kwa Allaah mpaka katika moyo wa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam), kama sivyo, basi bila shaka imechukuliwa kutoka katika Aayah iliopita:

وَيَتَّبِعْ غَيْرَ سَبِيلِ الْمُؤْمِنِينَ

"... na akaifuata njia isiyokuwa ya Waumini... " **(an-Nisaa 04 : 115)**

Kwa hivyo, ikiwa kwa yule mwenye: "Kumpinga Mtume" na "akafuata njia isiyokuwa ya Waumini" ametahadharishwa na Moto, kinyume chake, ni kwamba yule mwenye kufuata "Njia ya waumini" - basi bila shaka kaahidiwa Pepo, na huu ndo ukweli.

Hivyo, Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alipojibu swali [alipoulizwa na Maswahabah wake]: "Ni lipi kundi lililookoka?". Akasema:

"Ni Jamaa'ah."

Kwa hivyo, Jamaa'ah ni kundi la Waislamu. Halafu kukaja katika upokezi mwingine ambao [upokezi huo] unaupa nguvu maana [Hadiyth] hii, bali imezidisha kuiweka wazi na bayana. Pale aliposema Mtume (´alayhis-Salaam) [kuhusiana na kundi lililookoka]:

"Ni yale ambayo mimi na Maswahabah zangu tumesimama juu yayo."

Hivyo "Maswahabah zangu", ndiyo "Njia ya waumini.”

Aliposema Ibn al-Qayyim (Rahimahu Allaah) katika maneno yaliotangulia, alipowataja "*... na Maswahaba zake*" alichukua hayo kutoka katika Aayah iliotangulia na Hadiyth hii.

Hali kadhalika ipo Hadiyth nyingine maarufu, Hadiyth ya al-'Irbaad Ibn Saariyah (Radhiya Allaahu 'anhu) ambayo pia nitaifupisha, ili tuache nafasi ya baadhi ya Maswali. Nukta yenyewe tuitakayo, ni pale aliposema Mtume (´alayhis-Salaam):

"Shikamaneni na Sunnah zangu na Sunnah za Makhalifah wangu waongofu baada yangu."

Hivyo, hapa [tunaona dalili hali kadhalika] ni kama ile Hadiyth ya kabla yake [tulioitaja] na Aayah iliotangulia [tulioitaja]. Hakusema Mtume (´alayhis-Salaam): "Shikamaneni na Sunnah zangu" tu, bali amezifungamanisha Sunnah zake na Sunnah za Makhalifah (wake) waongofu.

Mpaka kufikia hapa sisi tunasema - na khaswa katika zama hizi ambazo zimejaa maoni mbali mbali, mifumo, madhehebu, na kumekithiri vipote na makundi, mpaka imekuwa vijana wengi wa Kiislamu wamekuwa wakiishi na wasi wasi, ikawa [kijana huyo] hajui ajinasibishe na kikundi kipi. Hapa kunakuja jibu kutokamana na Aayah na Hadiyth mbili tulizozitaja. Fuata Njia ya waumini! Njia ya waumini (Maswahabah) zama zetu wapo? Jibu ni hapana, bali walikuwa katika zama za kwanza - zama za Maswahabah - Salaf-us-Swaalih (wema waliotangulia). Hawa watu ndio inatakikana

wawe ni *Qudwah* kwetu na tuchukue mfano kwao, na wala hakuna kabisa asiyekuwa wao katika uso wa ardhi (ambao twafaa kuwaiga).

Kwa hivyo, hiki ndio kiini na nukta yenyewe, Da´wah yetu imejengeka juu ya nguzo tatu: juu ya:

1) Qur-aan,
2) Sunnah, na
3) Kuwafuata Salaf-us-Swaalih.

Hivyo basi, yeyote anayedai ya kwamba anafuata Qur-aan na Sunnah na wala hawafuati Salaf-us-Swaalih, na akawa anasema (kwa majigambo) kwa hali ya maneno na vitendo vyake:

"*Wao ni wanaume na sisi pia ni wanaume*"

Basi mtu huyu atakuwa katika upindaji na katika upotevu kabisa. "Wao ni wanaume na sisi ni wanaume", basi mtu huyu atakuwa katika upindaji na katika upotevu kabisa. Kwa nini iwe hivyo? Kwa sababu hakuchukua dalili ambazo tumetoka kuwatajia karibu. Je, huyu kafuata "Njia ya waumini?" Hapana! Je, huyu amewafuata Maswahabah wa Mtume Mtukufu? Hapana! Kafuata nini sasa? Ikiwa hakufuata matamanio yake, basi atakuwa amefuata akili yake. Na je, akili imesalimika na kukosea? Jibu ni "hapana." Kwa hivyo, atakuwa amepotea upotofu ulio wazi. Mimi naamini ya kuwa sababu za kutofautiana nyingi zilizorithiwa katika vipote maarufu sawa vya zamani, na tofauti zilizozagaa nyingi leo, ni [watu] kukosa kurudi katika asli hii ya tatu, nayo (watu kufuata Qur-aan na Sunnah kwa ufahamu wa) Salaf-us-Swaalih.

Kila mmoja wetu anadai ya kwamba anafuata Qur-aan na Sunnah, na ni mara ngapi tumesikia maneno mfano wa haya kwa vijana waliochanganyikiwa, Pindi wanaposema:

"*Ewe ndugu, watu hawa wanasema pia ya kwamba wanafuata Qur-aan na Sunnah, na hawa wengine pia wanasema wanafuata Qur-aan na Sunnah*".

Hivyo, cha kumaliza ugomvi ni kipi?

Ni (mtu) kufuata Qur-aan na Sunnah na Manhaj (mfumo) wa Salaf-us-Swaalih. Yule atakayefuata Qur-aan na Sunnah bila ya kutegemea juu ya (ufahamu wa) Salaf-us-Swaalih, basi hajafuata kweli Qur-aan na Sunnah, bali atakuwa amefuata akili yake tu

kama sitosema matamanio yake. Kutokana na kawaida yangu, nitawapa baadhi ya mifano ili niwawekee wazi masuala haya zaidi, bali asli hii muhimu, nayo ni: (Mtu kufuata Qur-aan na Sunnah) kwa Manhaj ya Salaf-us-Swaalih.

Kuna maneno yaliyopokelewa kutoka kwa al-Faaruuq 'Umar Ibn al-Khattwaab (Radhiya Allaahu 'anhu), anasema:

**"Wakiwajadili Ahl-ul-Ahwaa wal-Bid´ah (watu wanaofuata matamanio yao na wazushi) kwa Qur-aan, basi jadiliana nao kwa Sunnah."**

Kwa nini 'Umar kasema maneno haya? Kwa ajili ya hili, ni pindi Aliposema Allaah (´Azza wa Jalla), Akimwambia Mtume Wake (´alayhi-Salaam):

وَأَنزَلْنَا إِلَيْكَ الذِّكْرَ لِتُبَيِّنَ لِلنَّاسِ مَا نُزِّلَ إِلَيْهِمْ

"Na Tumekuteremshia Adh-Dhikra (Qur-aan ee Muhammad صلى الله عليه وآله وسلم) ili uwabainishie watu (kwa Sunnah) yaliyoteremshwa... " **(an-Nahl 16 : 44)**

Je, Muislamu anaweza, ambae ni mfasaha wa lugha ya kiarabu - kama wasemavyo *Sibawayh* wa zama hizi mwenye ujuzi wa lugha ya kiarabu na sarufi zake, kuweza kuifahamu Qur-aan bila ya kuitumia njia ya Mtume wetu (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam)? Jibu ni hapana! La sivyo, ndio maana ya Kauli Yake Allaah (Ta´ala):

"... ili uwabainishie watu (kwa Sunnah) yaliyoteremshwa... " **(an-Nahl 16 : 44)**

Kauli Yake hii ingekuwa haina maana yoyote? Kamwe, ni jambo lisilowezekana katu Maneno ya Allaah yakawa hayana maana yoyote. Hivyo basi, mtu yeyote mwenye kutaka kuifahamu Qur-aan bila ya kupitia njia isiyokuwa ya Mtume (´alayhis-Salaam) - yaani Sunnah - basi huyo amepotea upotevu wa wazi. Isitoshe, kuna uwezekano wa mtu huyo, akaweza kuifahamu Qur-aan na Sunnah kwa kupitia njia nyengine isiyokuwa njia ya Maswahabah wa Mtume (´alayhis-Salaam)? Jibu hali kadhalika ni hapana! Hili kwa sababu wao (Maswahabah) ndio waliotusimulia - jambo la kwanza, lafdhi (matamshi) ya Qur-aan ambayo Kaiteremsha Allaah kwenye moyo wa Muhammad (´alayhis-Salaam). Na la pili, wao ndio wametusimulia bayana yake Mtume (´alayhis-Salaam) iliotajwa katika Aayah iliyotangulia, na utekelezaji wake Mtume (´alayhis-Salaam) wa kimatendo wa hii Qur-aan Tukufu. Ufafanuzi wake Mtume (´alayhis-Salaam) wa Qur-aan unaweza kuwa katika vigawanyo vitatu: [1] Maneno, [2] Vitendo na [3], Taqriyr (kuruhusu au kukubali kitu kwa hali ya kukinyamazia).

Ni kina nani waliotusimulia kuhusu maneno yake Mtume (´alayhis-Salaam)? Ni Maswahabah zake. Ni kina nani waliotusimulia kuhusu vitendo vyake Mtume (´alayhis-Salaam)? Ni Maswahabah zake. Ni kina nani waliotusimulia kuhusu kulinyamazia kwake jambo (kwa hali ya kuliruhusu na kulikubali)? Ni Maswahabah zake. Kwa ajili hii, ni jambo lisilowezekana kwetu, tukaifahamu Qur-aan na Sunnah - kwa ubingwa wetu wa kilugha tu. Bali ni lazima kwetu kutafuta msaada kwa hilo (kuifahamu Qur-aan). Lakini hii haimaanishi ya kwamba lugha hatuwezi kuihitajia katu (katika kuifahamu Qur-aan), hapana. Na kwa hili, sisi tunaamini ya kwamba ´Aajiym (wale wasiokuwa waarabu) ambao hawajui lugha ya kiarabu vizuri, hutumbukia katika makosa mengi mno. Na khaswa huzidi hutumbukia katika kosa hili la msingi, nako ni kwa kule kutorudi kwao katika ufahamu wa Salaf-us-Swaalih katika kuifahamu Qur-aan na Sunnah. Mimi simaanishi kwa maneno yangu niliyoyasema hapo nyuma ya tusiipe lugha (ya kiarabu) umuhimu kabisa (katika kuifafanua Qur-aan). Itakuwaje? Kwani tukitaka kuyafahamu maneno ya Maswahabah basi bila shaka ni lazima tuifahamu lugha ya kiarabu, kama jinsi ambavyo kadhalika ili tuweze kuifahamu Qur-aan na Sunnah, inamlazimu mtu ajue lugha ya kiarabu.

Kwa hivyo sisi tunasema, ya kuwa bayana ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) iliotajwa katika Aayah iliotangulia, imegawanyika katika mafungu matatu: Maneno yake, vitendo vyake na Taqriyr (kulinyamazia kwake jambo). Tutachukua mfano katika kuwabainishia ya kuwa vigawanyo hivi ni jambo lililothibiti, na halina kipingamizi chochote. Ni Kauli Yake Allaah (Tabaaraka wa Ta´ala):

وَالسَّارِقُ وَالسَّارِقَةُ فَاقْطَعُوا أَيْدِيَهُمَا

"Mwizi mwanamume na mwizi mwanamke, wakateni mikono yao." **(al-Maaidah 05 : 38)**

Hebu angalia sasa, jinsi vipi hatuwezi kuitegemea katika kuifahamu Qur-aan kwa kutumia lugha. Mwizi kilugha ni mtu yeyote ambaye ameiba mali kutoka sehemu fulani, sawa kitu hicho kikiwa hakina thamani yoyote, inaweza kuwa yai kwa mfano au mkate. Ikiwa ataiba hivi kilugha atahesabika kuwa ni mwizi. Anasema Allaah (Ta´ala):

وَالسَّارِقُ وَالسَّارِقَةُ فَاقْطَعُوا أَيْدِيَهُمَا

"Mwizi mwanamume na mwizi mwanamke, wakateni mikono yao." **(al-Maaidah 05 : 38)**

Je, ni kila mwenye kuiba ni wajibu ukatwe mkono wake? Jibu ni hapana. Kwanini? Ni kwa sababu yule mwenye kubainisha (yaani Mtume) ambae ni juu yake kulibainisha lile jambo linaloelezwa (yaani Qur-aan), mwenye kubainisha ni Mtume wa Allaah, na kinachobainishwa ni Qur-aan; ametubainishia Mtume wa Allaah ni nani anayestahiki kukatwa mkono miongoni mwa wezi. Akasema Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam):

"Msiukate mkono isipokuwa kwa (mwenye kuiba) robo ya dinari na zaidi ya hapo."

Kwa hivyo mwenye kuiba kitu chenye thamani chini ya robo dinari - hata kama kilugha ataitwa mwizi, lakini mtu huyu Kishari´ah haitwi mwizi. Sasa hapa, tunakuja kwenye uhakika wa kielimu, jambo ambalo wengi katika watafutaji wa elimu wameghafilika kwacho. Tuna lugha ya kiarabu ambayo inarithiwa, na tuna lugha ya Kishari´ah, ambayo Allaah (Ta´ala) ndie Aliyeipa jina hilo na kuieleza. Hawakuwa waarabu ambao walikuwa wakizungumza kwa lugha hiyo ya Qur-aan ambayo ndiyo lugha imeteremshwa na Qur-aan - walikuwa hawajui istilaha kama hii (yakuitwa mwizi, mwenye kuiba chini ya robo dinari). Inaposemwa mwizi kilugha, basi anaingia humo kila aina ya mwizi. Ama kunaposemwa mwizi Kishar´iah, haingii kila mwizi, bali ni yule ambaye kaiba robo dinari au zaidi ya hapo. Basi huu ni mfano tumeutaja ya kwamba hatuwezi kutegemea kwa kuifahamu Qur-aan na Sunnah kwa ujuzi wetu lugha ya kiarabu peke yake. Haya ni makosa ambayo hutumbukia wengi katika waandishi wa zama hizi. Hutanguliza ujuzi wao wa lugha ya kiarabu kabla ya Aayah za Qur-aan na Hadiyth za Mtume (´alayhis-Salaam). Hivyo wakavifasiri, wakatuletea tafsiri za Bid´ah, wasizozijua waislamu wa hapo kabla.

Kutokana na hili, tunasema, ni wajibu kufahamu ya kwamba Da´wah ya Kiislamu ya haki imejengeka juu ya misingi mitatu:

1) Qur-aan,
2) Sunnah, na
3) Kwa ufahamu wa Salaf-us-Swaalih.

Kwa hivyo, usiifasiri Aayah hii:

"Mwizi mwanaume na mwizi mwanamke... "

kulingana lugha kama jinsi ilivyo; bali yatakikana kuifasiri kwa mujibu wa lugha ya Kishari´ah; ambapo alisema Mtume (´alayhis-Salaam):

"Msiukate mkono isipokuwa kwa (mwenye kuiba) robo ya dinari na zaidi ya hapo."

Mwisho wa Aayah Kasema (Allaah):

"... wakateni mikono yao." **(al-Maaidah 05 : 38)**

Mkono ni upi kilugha? Huu wote ni mkono - kuanzia ncha za vidole hadi kwenye makwapa - wote huu ni mkono. Je, unaweza kukatwa kuanzia hapa, au hapa, au hapa au hapa? Kabainisha hilo Mtume (´alayhis-Salaam) kwa vitendo vyake. Hakuna Hadiyth Swahiyh - kama ile iliyothibiti ni mwizi upi anayestahiki kukatwa mkono wake - hatuna Hadiyth inayowekea mpaka wazi wazi kwa kubainisha kwa kauli yake ni kuanzia wapi mtu inafaa akatwe, isipokuwa tuko na bayana yake ya kimatendo kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam). Ni kutoka wapi tumejua utendaji huu? Ni kutoka kwa Salaf-us-Swaalih - Maswahabah wa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam). Hili ni fungu la pili, nalo ni bayana ya kimatendo.

Fungu la tatu ni kuruhusu kwa Mtume (´alayhis-Salaam) kwa jambo ambalo halipingi, na wala halikatazi (akalinyamazia). Kuruhusu huku si kwa njia ya maneno kutoka kwake wala kitendo alichokifanya yeye; bali kitendo hichi kimetendwa na mtu mwengine, kila alipokiona (Mtume - ´alayhis-Salaam) alikiruhusu na kukiunga mkono. Ina maana, anapoona jambo (Mtume) akalinyamazia na kuliruhusu, inakuwa ni jambo la kuruhusiwa na lenye kujuzu. Na akiona jambo fulani na akalipinga, na lau hata kama jambo hilo lilifanywa na baadhi ya Maswahabah zake, lakini imethibiti kutoka kwake ya kwamba amelikataza, basi haya ambayo ameyakataza yatakuwa na nguvu juu ya yale aliyoyaruhusu (kwa kuyanyamazia). Nitawapa mfano wa haya mambo mawili kutokana na Hadiyth.

Amesema 'Abdullaah bin 'Umar Ibn al-Khattwaab (Radhiya Allahu 'anhu):

"Tulikuwa tukinywa hali ya kuwa tumesimama, na tukila nasi huku twatembea katika wakati wa uhai wa Mtume (´alayhis-Salaam)."

Kaelezea 'Abdullaah katika Hadiyth hii mambo mawili: [1] Kunywa kwa kusimama, na [2] kula huku watembea. Na kasema ya kwamba haya ni mambo mawili yalifanywa katika zama za Mtume (´alayhis-Salaam). Sasa ni ipi hukumu ya Kishari´ah kuhusiana na masuala haya mawili, kunywa kwa kusimama na kula huku watembea? Tukitumia maneno (vipimo) vilivyotangulia tutaweza kuchukua hukumu - bila ya shaka - pamoja na mahitaji yasiyokuwa na budi, nayo ni mtu awe na elimu (ujuzi) kwa aliyokuwemo Mtume wa Allaah (´alayhis-Salaam) - kwa kutamka, kimatendo na Taqriyr.

Tunaporejea katika Sunnah Swahiyh, kuhusiana na jambo la kwanza (kunywa kwa kusimama), jambo ambalo wamepewa kwalo mtihani idadi kubwa ya waislamu, kama

si wengi katika waislamu kwa kwenda kinyume na kauli ya Mtume Mtukufu, nako ni kunywa kwa kusimama. Walikuwa wakinywa kwa kusimama, wakivaa (yaani wanaume) dhahabu, walikuwa wakivaa hariri. Huu ni ukweli usiopingika. Lakini je, Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) aliyakubali hayo? Jibu ni kuwa, alikataza baadhi ya mambo na akakubali baadhi ya mambo. Kwa hivyo, alichokikataza kikaingia katika mipaka ya Munkar (maovu), na alichokiruhusu kikaingia katika mipaka ya Ma'ruuf (vizuri). Sasa amekataza kunywa kwa kusimama katika Ahaadiyth nyingi. Kuna Hadiyth nyingi na wala sitaki kuziingia humo tusije kutoka katika mada... Lakini itatosheleza kuwapa Hadiyth moja Swahiyh iliyosimuliwa na Imaam Muslim kutoka katika Swahiyh yake, Hadiyth kutoka kwa Anas Ibn Maalik (Radhiya Allaahu 'anhu) aliyesema:

"Kakataza Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) kunywa kwa kusimama."

Katika upokezi mwingine, kasema:

"Kazuia Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) kunywa kwa kusimama."

Hivyo, jambo hili ambalo lilikuwa likifanywa - kama alivyosema Ibn ´Umar - wakati wa uhai wa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam), kalikataza Mtume. Kwa hivyo, jambo walilokuwa wakilifanya ni jambo limekatazwa, kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kulikataza. Lakini sehemu ya pili ya Hadiyth (ya Ibn 'Umar) isemayo ya kwamba walikuwa wakila na huku wanatembea, hawakupata khabari zozote za makatazo kutoka kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam). Wakachukua kutokana na ukimya huo kuwa ni hukumu ya Kishari´ah ya (kujuzu kwa jambo hilo). Mpaka hapa, tumekuja kujua wazi ilivyokuwa umuhimu wa kufahamu Qur-aan na Sunnah kwa waliokuwemo Salaf-us-Swaalih, na si kwa mtu yeyote kutosheka na kufahamu Qur-aan na Sunnah kwa ufahamu wa elimu yake, nisiseme kwa ujinga wake.

Baada ya kuibainisha muhimu wa jambo hili "kwa Manhaj ya Salaf-us-Swaalih", niwape baadhi ya mifano.

Zamani Waislamu waligawanyika katika mapote mengi; umeshawasikia Mu'tazilah, umeshawasikia Murji-ah, umeshawasikia Khawaarij, umeshawasikia Zaydiyyah, bila ya kuwasahau Shiy´ah Raafidhwah na makundi mengine. Hakuna katika watu hawa pote - licha ya upotevu mkubwa watakaokuwa nao - wanakosa kushiriki pamoja kama jinsi wanavyosema waislamu wengine, nao wanasema:

"*Sisi tupo juu ya Qur-aan na Sunnah.*"

Hakuna yeyote asemaye: "Sisi hatufuati Qur-aan na Sunnah." Na lau mmoja wao atasema hivyo, atakuwa ametoka katika Uislamu kabisa. Hivyo, migawanyiko yote hii ya nini maadamu wote wanategemea Qur-aan na Sunnah - na mimi nashuhudia ya kwamba wanategemea Qur-aan na Sunnah. Lakini huku ni kutegemea (kufuata) kivipi, bila ya kutegemea juu ya asli ya tatu, ambayo ni kwa waliokuwemo Salaf-us-Swaalih?! Pamoja na nukta nyingine ambayo ni lazima kuikumbusha - nayo ni kwamba Sunnah ni tofauti kabisa na Qur-aan Tukufu, kwa maana ya kwamba Qur-aan Tukufu ni yenye kuhifadhiwa baina ya magamba mawili ya misahafu, kama inavyojulikana kwa watu wote. Ama Sunnah, jambo la kwanza imeenea katika mamia ya vitabu, kama sio maelfu ya vitabu, ambavyo miongoni mwavyo kuna idadi kubwa yake bado ingali katika ulimwengu wa maficho (yaani vitabu hivyo vipo lakini bado havijachapishwa na kuenea). Isitoshe jengine, hata hivi vitabu ambavyo baadhi yavyo vipo katika uchapishwaji leo, kuna vile vitabu ambavyo (vina Ahaadiyth) Swahiyh na kuna (vya Ahaadiyth) dhaifu. Wale wanaotegemea Sunnah - sawa ikiwa wao ni katika Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa'ah kwa Manhaj ya Salaf-us-Swaalih au wakawa ni katika makundi mengine, wengi katika watu hawa hawawezi kutofautisha baina ya Sunnah (Hadiyth) Swahiyh na Sunnah (Hadiyth) dhaifu. Kwa hivyo hatimae wanatumbukia katika kukikhalifu (kwenda kinyume) na Qur-aan na Sunnah kwa sababu ya kutegemea kwao kwa Ahaadiyth dhaifu na ma´udhuu' (za kutungwa).

Nukta tuitakayo, ni kwamba kuna baadhi ya makundi ambayo tumeyaashiria yanapinga uhakika wa Qur-aan na Hadiyth (Swahiyh) za Mtume, zamani na hata mpaka sasa (wapo). Qur-aan Tukufu inathibitisha na kuwabashiria waumini kuhusiana na neema kubwa sana watakayoipata siku ya Qiyaamah, siku ambayo watakutana na Mola wao (´Azza wa Jalla) Peponi. Na hapo ni pale Mola wa walimwengu Atapojitokeza kwao, watamuona. Kama alivyosema hilo mwanachuoni mmoja as-Salafiy:

**"Waumini watamuona (Mola wao), bila ya Kayf (kuulizia) itakuwaje na Tashbiyh (kufananiza itavyokuwa) na kulitolea mifano yake (ya namna Atakavyokuwa)."**

Hili (la kumuona Allaah) lina dalili katika Qur-aan na mamia ya nususi ya Ahaadiyth za Mtume (alayhis-Salaam). Inakuweje basi wakapinga neema hii baadhi ya makundi ya zamani na ya sasa?! Ama katika makundi ya zamani (yanayopinga hilo) ni Mu'tazilah. Leo, kutokana na ninavyojua hakuna katika uso wa ardhi anaesema: "Sisi ndio Mu'tazilah", "Sisi ´Aqiydah yetu ni ya Mu´tazilah." Lakini mimi, nimemuona mtu mmoja mpumbavu aliyejitangaza wazi wazi na kusema ya kwamba yeye ni Mu'taziliy. Na anakanusha mambo mengi ya kweli, kwa sababu yeye alikuwa ni mtu wa kuvamia tu. Sasa hawa Mu'tazilah wameipinga neema hii na wakasema kwa kutumia akili zao

dhaifu: "Ni jambo lisilowezekana Akaonekana Allaah (´Azza wa Jalla)!" Je, wamefanya nini? Wameikataa Qur-aan? Allaah Anasema katika Qur-aan Tukufu:

وُجُوهٌ يَوْمَئِذٍ نَّاضِرَةٌ إِلَى رَبِّهَا نَاظِرَةٌ

"Zipo nyuso siku hiyo zitaong´ara, zinamwangallia Mola Wao." **(al-Qiyaamah 75 : 22-23)**

Je, wameikataa Aayah hii? Hapana, hawakuikataa, hawakukufuru wala kuritadi. Lakini mpaka hivi leo, Ahl-us-Sunnah wa kikweli wanawahukumu Mu'tazilah ya kwamba ni wapotevu, lakini hawawatoi katika duara la Uislamu. Kwa sababu wao hawaipingi Aayah hii, bali wamepinga maana yake ya haki ambayo imekuja bayana yake katika Sunnah, kama ambavyo tutakumbusha. Allaah (´Azza wa Jalla) Aliposema kwa haki ya waumini wataoingia Peponi:

وُجُوهٌ يَوْمَئِذٍ نَّاضِرَةٌ إِلَى رَبِّهَا نَاظِرَةٌ

"Zipo nyuso siku hiyo zitakazong´ara, zinamwangalia Mola Wao." **(al-Qiyaamah 75 : 22-23)**

Kwa hivyo wao wakabadilisha maana yake - wameiamini lafdhi (maneno ya Aayah) hii, na wakakanusha maana yake. Na lafdhi kama wasemavyo wanachuoni ndio makusudio ya maana yenyewe. Tukiamini lafdhi (matamshi) lakini tusiamini maana yake, basi imani hii huwa haina faida yoyote. Lakini kwanini watu hawa wamekanusha kuonywa kwa Allaah (siku ya Qiyaamah)? Ni kutokana na akili yao mbovu, wasije kufikiria na kudhania ya kwamba mja huyu, aliyeumbwa na aliye na sifa ya mapungufu hana uwezo wa kumuona Allaah (´Azza wa Jalla) wazi wazi (Aakhirah). Kama jinsi Mayahudi walivyomuomba Muusa (wamuone Allaah Duniani), basi Allaah Akawakatalia - kama ilivyo katika kisa maarufu:

وَلَـكِنِ انظُرْ إِلَى الْجَبَلِ فَإِنِ اسْتَقَرَّ مَكَانَهُ فَسَوْفَ تَرَانِي

"Lakini utazame huo mlima. Ukibaki pahala pake basi utaniona." **(al-A´araaf 07 : 143)**

Akili zao finyu kiasi ya kwamba wakajihisi ya kwamba wamelazimika kuichezea dalili ya Aayah ya Qur-aan na wakawa tayari kuibadilisha maana yake. Kwanini? Hii ni kwa sababu imani zao kuamini mambo ya Ghayb (yaliyojificha) ni dhaifu, na imani zao wanavyoziamini akili zao zina nguvu zaidi kuliko imani yao katika mambo ya Ghayb, ambayo tumeamrishwa kwayo, katika mwanzo wa Suurat al-Baqarah:

الم ذَٰلِكَ الْكِتَابُ لَا رَيْبَ ۛ فِيهِ ۛ هُدًى لِّلْمُتَّقِينَ

" Alif Laam Miym. Hiki ni Kitabu kisicho na shaka ndani yake, ni Hidaaya (uongofu) kwa wenye taqwa (wachajiAllaah)." **(al-Baqarah 02 : 01-02)**

Ni kina nani hao?

بِالَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِالْغَيْ

"Ambao huamini ya ghayb." **(al-Baqarah 02 : 03)**

Ni katika Sifa za Allaah kuu ni Yeye kutookekana, kwa hivyo kila wakati Mola wetu Anapojielezea Mwenyewe, ni juu yetu kusadikisha kumuamini kwa kuwa akili zetu ni pungufu sana. Mu'tazilah hawakubaliani na ukweli huu, na ndio sababu ya wao kupinga ukweli mwingi uliothibiti katika Shari´ah, miongoni mwa waliyoyapinga ni Kauli Yake (Tabaaraka wa Ta´ala)

وُجُوهٌ يَوْمَئِذٍ نَّاضِرَةٌ إِلَى رَبِّهَا نَاظِرَةٌ

"Zipo nyuso siku hiyo zitakazong´ara, zinamwangalia Mola Wao." **(al-Qiyaamah 75:22-23)**

Hali kadhalika katika Aayah nyingine - na huenda ikawa imefichikana zaidi kwa watu hawa kuliko Aayah ya mwanzo; nayo ni Kauli Yake Allaah (´Azza wa Jalla):

لِّلَّذِينَ أَحْسَنُوا الْحُسْنَىٰ وَزِيَادَةٌ

"Kwa wale waliofanya ihsaan watapata (jazaa ya ihsaan; nayo ni) al-Husnaa (Pepo) na zaidi (ya hayo ni kupata taadhima ya kumuona Allaah)." **(Yuunus 10 : 26)**

"al-Husnaa" yaani watapata Pepo, na "az-Ziyaadah" yaani ni kumuona Allaah huko Aakhirah. Namna hii ndio zimekuja (zimethibiti) Hadiyth katika Swahiyh Muslim na upokezi Sahihi Hadiyth kutoka kwa Sa'd Ibn Abiy Waqqaas (Radhiya Allaahu 'anhu) kasema, Amesema Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam):

"Kwa wale waliofanya ihsaan watapata (jazaa ya ihsaan; nayo ni) "al-Husnaa" - watapata Pepo; wa "Ziyaadah", kumuona Allaah."

Hawa Mu'tazilah na pia Shiy´ah wamepinga, ambao ni Mu'tazilah katika ´Aqiydah zao, wamepinga kumuona Allaah, jambo ambalo limethibiti katika Aayah ya kwanza na likabainishiwa na Mtume wa Allaah (´alayhis-Salaam) katika Aayah ya pili. Pamoja na

kuthibiti Ahaadiyth Mutawaatir kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) kuhusu kumuona Allaah, wakatumbukia katika Ta'wiyl yao (kupotosha maana sahihi) ya Qur-aan katika kuzipinga Ahaadiyth zilizo Swahiyh kutoka kwa Mtume (´alayhis-Salaam). Wakawa wamejiondoa kutoka katika kundi lililookoka, (kama alivyosema Mtume):

"Ni lile lililokuwemo katika yale niliomo mimi na Maswahabah zangu."

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alikuwa juu ya imani - akiamini ya kwamba waumini watamuona Mola wao, kwa sababu imepokelewa katika Swahiyh mbili (al-Bukhaariy na Muslim) Hadiyth kutoka kwa kundi kubwa la Maswahabah wa Mtume (´alayhis-Salaam), kwa mfano miongoni mwao kuna Abu Sa'iyd al-Khudhriy, Anas Ibn Maalik - na licha ya vitabu hivyo Swahiyh viwili - kuna Abu Bakr Asw-Swiddiyq n.k. Kasema Mtume (´alayhis-Salaam):

"Kwa hakika nyinyi mtamuona Mola wenu siku ya Qiyaamah, kama vile muuonavyo mwezi katika usiku (ung'arao) wenye mwezi mpevu - hamtasongamana katika kumuona."

Na makusudio maana yake, ni kwamba hamtokuwa na matatizo (kusongamana) katika kumuona Allaah, kama jinsi hamna matatizo yoyote katika kuuona mwezi Laylat-ul-Badr (ambapo mwezi unakuwa mkubwa), kunakuwa hakukutanda mawingu. Wamezipinga Ahaadiyth hizi kulingana na akili zao chafu, kwa hivyo wakawa ni madhaifu wa imani. Huu ni mfano mmoja wa mambo ambayo wametumbukia humo baadhi ya vipote vya zamani, na pia baadhi ya vipote vya leo, kama vile Khawaarij, na miongoni mwao (Khawaarij) ni hawa Maibadhi (Ibaadhiy) ambao hivi leo wamekuwa washupavu kwa kulingania watu katika upotevu wao. Wamekuwa na makala na vitabu wanavyovisambaza na kuvieneza, na wanahuisha upotevu wa Khuruuj (uasi) jambo ambalo linajulikana kwa Khawaarij tangu zamani katika kupinda kwao - miongoni mwa upotevu huo ni kupinga kwao kuonekana kwa Allaah (´Azza wa Jalla) Peponi.

Sasa tutawaletea mfano tulionao leo, Qadiyani. Huenda ushawahi kuwasikia. Watu hawa wanasema kama tunavyosema sisi: "*Nashuhudia ya kwamba hapana mola anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah, na kwamba Muhammad ni Mtume wa Allaah.*" Wanaswali Swalah tano, wanasimamisha Swalah ya Ijumaa, wanafanya Hajj katika nyumba tukufu na wanafanya 'Umrah. Lakini wanatofautiana na sisi katika mambo mengi ya ´Aqiydah. Miongoni mwa mambo hayo ni kusema kuamini kwao ya kwamba mlango wa Utume haujafungwa (haukumalizika). Wanaamini ya kwamba watakuja Manabii baada ya Muhammad (´alayhis-Salaam) na wanadai ya kwamba tayari mmoja wao ameshakuja kwa Qadiyani katika mji ulioko India. Kwa hivyo (kutokana na imani

yao) ni kwamba yeyote ambae hamuamini Mtume huyu, basi ni Kafiri. Vipi wanaweza kusema hivyo, pamoja na kuwa Aayah iko wazi:

مَّا كَانَ مُحَمَّدٌ أَبَا أَحَدٍ مِّن رِّجَالِكُمْ وَلَكِن رَّسُولَ اللهِ وَخَاتَمَ النَّبِيِّينَ

"Muhammad si baba wa yeyote katika wanaume wenu, bali ni Mtume wa Allaah na Mwisho wa Manabii." **(al-Ahzaab 33 : 40)**

Vipi wataleta madai haya, pamoja na kuwa kuna Ahaadiyth nyingi Mutawaatir zikisema:

"Hakuna Mtume mwengine baada yangu."

Kwa hivyo wakabadilisha maana ya Qur-aan na Sunnah, na hawakufasiri Qur-aan na Sunnah kama walivyovifasiri Salaf-us-Swaalih. Na waislamu nao pia wakawafuata kwa hilo bila ya khilaaf baina yao, mpaka alipokuja huyu mpotevu, aitwae Mirzah Ghulaam Ahmad al-Qadiyaaniy, akadai ya kwamba ni Nabii. Na ana kisa kirefu, hatuwezi hivi sasa kukiingia. Basi akawadanganya watu wengi wasiokuwa na elimu ya ukweli huu, (elimu) ambayo humuhifadhi Muislamu asipotee ikawa anaenda kuliani na kushotoni, kama walivyopotezwa Qadiyani na mtu huyu Dajjaal (Shaytwaan) aliyedai Utume.

Walifanya nini na Aayah hii:

وَلَكِن رَّسُولَ اللَّهِ وَخَاتَمَ النَّبِيِّينَ

"... bali ni Mtume wa Allaah na Mwisho wa Manabii." **(al-Ahzaab 33 : 40)**

Wakasema maana yake si kwamba hakuna Mtume baada yake, maana ya "Khaatam" ni pambo la Mitume, kama ambavyo "Khaatam" ni pambo la kidole, basi hali kadhalika Muhammad ni pambo la Mitume. Hivyo, nao pia hawakuikanusha Aayah. Hawakusema Aayah hii Hakuiteremsha Allaah kwenye moyo wa Muhammad. Lakini wamekufuru kutokana na maana yake ya kiuhakika. Sasa nini inafidisha imani ya kutamka bila ya imani ya uhakika wa mambo.

Ikiwa ukweli huu wewe huna shaka nao, basi ni njia ipi itakayokufanya kuweza kufikia kufahamu ukweli wa maana ya Qur-aan na Sunnah. Tayari mmekwishaijua njia. Si juu yetu kuitegemea elimu yetu tu ya lugha tukaifasiri Qur-aan na Sunnah kwa

matamanio yetu, au kwa ada zetu, Taqliyd, au kufuata kwetu madhehebu, au kwa njia zetu, bali ni kama tulivyosema, na nitahitimisha maneno yangu kwa kauli hii:

***"Na kila kheri inapatikana kwa kuwafuata Salaf (wema waliotangulia), na kila shari inapatikana kwa kuzua Khalaf (waliokuja baadae)."***

Huenda kwa haya machache:

إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَذِكْرَىٰ لِمَن كَانَ لَهُ قَلْبٌ أَوْ أَلْقَى السَّمْعَ وَهُوَ شَهِيدٌ

"Hakika katika hayo upo ukumbusho kwa mwenye moyo au akatega sikio naye yupo anashuhudia." **(Qaaf 50 : 37)**[1]

***Swalla Allaahu ´alaa Muhammad, wa ´alaa aalihi wa Aswhaabihi wa sallam.***

[1] *Chanzo cha mawaidha haya kiarabu:* ***http://www.alalbany.ws/alalbany/huda_noor_audio/640.rm***
*Mawaidha haya yamefasiriwa pia kwa njia ya video: 1)* ***http://youtu.be/QUFLQ3Leg3s*** *& 2)* ***http://youtu.be/ZY1daphoPsU***